# Yesu ni Mungu!!!

## Na Willy Emmanuel Yudah

**Karibu mpenzi msomaji katika jarida la "Asomaye na Afahamu". Leo nitajikita katika mada inayozungumzia Uungu wa Yesu. Yapo madhehebu ambayo hayaamini kuwa Yesu ni Mungu wakiwemo na rafiki zetu Waislamu. Leo nitaanza na madhehebu ya Kikristo yanayokanusha Uungu wa Yesu.**

**Karibu….**

Biblia haijawahi kuandika kwamba Yesu alisema "mimi ni Mungu". Hata hivyo hiyo haimaanishi kuwa Yesu hajawahi kudai kwamba yeye ni Mungu. Kwa mfano, chukua maneno ya Yesu katika Yohana 10:30;

**"Mimi na Baba tu umoja"**

Ili ujue maana ya maneno hayo aliyoyatamka Yesu, tazama walichofanya Wayahudi walipoyasikia hayo maneno.

"Basi wayahudi wakaokota mawe tena ili wampige.Ysu akawajibu, Kazi njema nyingi nimeowaonyesha zitokazo kwa Baba; kwa ajili ya kazi ipi kati ya hizo mnanipiga kwa mawe?" mstari wa 31-32

Tazama jibu lao kwa Yesu kuhusu sababu wanayotaka kumpigia;

"….Kwa ajili ya kazi njema hatukupigi kwa mawe; bali kwa kukufuru, na kwasababu wewe uliye mwanadamu, wajifanya mwenyewe u Mungu."

Wayahudi waliuelewa vizuri mstari wa 30 alichokuwa anamaanisha Yesu, alikuwa anamaanisha kuwa yeye ni Mungu! Aliposema mimi na Baba tu umoja (I and father are one sio I and Father are in unity bali one) alimaanisha kuwa yeye na Baba asili yao ni moja!

Mfano mwingine ni Yohana 8:58 Yesu aliposema;

"….Amin, Amin, nawambia, Yeye Ibrahimu asijakuwako, **mimi niko"** Wayahudi kwanini waliokota mawe? Soma Walawi 24:16. "Na yeye atakayelikufuru jina la BWANA hakika atauawa; mkutano wote watamuua kwa kumpiga kwa mawe;.." Je Yesu alimaanisha nini aliposema mimi niko hata wakaona amekufuru? Hebu tuone niko ni jina la nani? Kutoka 3:13-14; "….Tazama, nitakapofika kwa wana wa Waisraeli na kuwaambia, Mungu wa baba zenu amenituma kwenu; nao wataniuliza, Jina lake n'nani? Niwambie nini? Mungu akamwambia Musa, MIMI NIKO AMBAYE NIKO…**MIMI NIKO** amenituma kwenu."

Kwa maneno rahisi, katika Yohana 8:58 Yesu alikuwa anasema “Kabla Ibrahimu asijakuwako mimi ni Mungu”

Yohana anatoa mkazo juu ya Uungu wa Bwana Yesu. “…Naye Neno alikuwako kwa Mungu**, naye Neno alikuwa Mungu**….Naye **Neno alifanyika mwili**, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa **Mwana pekee atokaye kwa Baba….”** Mistari hii inaonyesha waziwazi kuwa Yesu ni Mungu.

Katika Matendo ya Mitume 20:28, Neno la Mungu linasema; “ Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha **kanisa lake Mungu alilolinunua kwa damu yake mwenyewe.** Ni nani aliyelinunua kanisa kwa damu yake mwenyewe? Siyo kwa damu bali kwa damu yake mwenyewe. Ni Yesu! Mathayo 16:18; 1 Timotheo 3:15, 1 Yohana 5:6; Waebrania 9:11-12; Waefeso 1:7

Kwa hiyo Yesu ni Mungu!

Tomaso alisema,

“Bwana wangu na Mungu!” Yohana 20:28

Na Yesu hakumkosoa kwamba amekosea. Tito 2:13 panatuhimiza kwa kusema

“tukilitazamia tumaini lenye Baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu, Mungu mkuu na mwokozi wetu;”

Tena, Katika Waebrania 1:8 twasoma,

“Lakini kwa habari za Mwana, asema, kiti chako cha enzi, Mungu, ni cha milele na milele. Na fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya adili”

Ukianza mstari wa tano utaona kuwa anayeongea Mungu Baba. Anapofika mstari wa 8 anamtaja Mwana kuwa Mungu! Ni nani na asimame anayeweza kukanusha na kusema Yesu siyo Mungu. Yesu ni Mungu!!! Isitoshe, tazama katika Ufunuo 19:10 ambapo malaika anamwelekeza Yohana kuwa anayestahili kusujudiwa ni Mungu lakini twaona ya kuwa Yesu alisujudiwa na hajwahi kukataa!

Mathayo 2:11 “Wakaingia nyumbani, wakamwona mtoto pamoja na Mariamu mamaye, wakaanguka wakamsujudia;”

Mathayo 14:33 “Nao walipokuwa ndani ya chombo wakamsujudia..”

Mathayo 28:9 “Na tazama, Yesu akakutana nao, akisema, Salamu! Wakakaribia, wakamshika miguu, wakamsujudia;”

Luka 24:52 “ Wakamwabudu; Kisha wakarudi Yerusalemu wenye furaha kuu”

Yohana 9:38 “Akasema, Naamini, Bwana, Akamsujudia”

Yesu hajawahi kuwakemea watu waliokuwa wanamsujudia au kumwabudu!!! Kama Yesu siyo Mungu, na angejua kuwa siyo Mungu, angewaambia watu wasimsujudie/kumwabudu kama malaika katika ufunuo alivyomwambia Yohana.

Zipo aya nyingi za maandiko matakatifu zinazothibitisha kuwa Yesu ni Mungu hata ukiona Isaya 9:6 kuhusu mwana akayezaliwa yaani Yesu “Mungu mwenye nguvu. Tena Mathayo 1:21-23, Yesu alitajwa kuwa Imanueli, Mungu pamoja nasi. Hadi hatua hii, bado huyamini maandiko yasemayo Yesu ni Mungu? Hii ni hatari!!!

Sababu kubwa inamfanya Yesu ahtibike kuwa Mungu ni kwamba, kama siyo Mungu, mauti yake isingetosha kulipa dhambi za ulimwengu “naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali kwa **dhambi za ulimwengu wote.** 1Yohana 2:2. Kama Yesu asingekuwa ni Mungu maana angekuwa ni kiumbe (aliyeumbwa) asingefaa kuwa sadaka dhambi zilizotendwa na wanadamu dhidi ya Mungu. Ni Mungu pekee anayeweza kuwa sadaka ya namna hiyo na ni Mungu pekee anayeweza kuipokea!

Mpendwa msomaji, mpaka hapa umeona kwa kuthibitisha katika maandiko ya kuwa Yesu ni Mungu. Kama vifungu vingine ambavyo vinakanusha Uungu wa Yesu, kwanza vitakuwa vinapingamana na hivi nilivyovitoa, Pili vitakuwa vinaifanya Biblia kuwa kitabu kinachojipinga. Haiwezekani! Aya zitakazopinga aya nilizotoa itabidi zitoke nje ya Biblia kwa sababu haiwezi kujipinga!